# BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA MAWASILIANO (TCRA CCC)

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI ZA WATUMIAJI ZA MIKOA

## JANUARI – MACHI 2024


*Aprili, 2024*

**1.0 JUMLA YA WATUMIAJI WALIOFIKIWA NA KAMATI**

| | IDADI YA WATU WALIOFIKIWA NA KAMATI ROBO YA TATU 2023/24 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **MKOA** | **KE** | **ME** | **WALEMAVU** | **JUMLA** |
| 1 | TABORA | 356 | 237 | 8 | 601 |
| 2 | ARUSHA | 226 | 302 | 89 | 617 |
| 3 | KIGOMA | 871 | 311 | 48 | 1230 |
| 4 | KUSINI PEMBA | 509 | 397 | | 906 |
| 5 | RUVUMA | 879 | 64 | 23 | 966 |
| 6 | TANGA | 678 | 787 | 74 | 1539 |
| 7 | MWANZA | 566 | 648 | 343 | 1557 |
| 8 | SIMIYU | 2161 | 377 | 12 | 2550 |
| 9 | MBEYA | 150 | 306 | 86 | 542 |
| 10 | MJINI MAGHARIB | 366 | 396 | 86 | 848 |
| 11 | IRINGA | 491 | 383 | | 874 |
| 12 | MOROGORO | 734 | 240 | | 974 |
| 13 | PWANI | 494 | 78 | 48 | 620 |
| 14 | MTWARA | 892 | 795 | 11 | 1698 |
| 15 | KAGERA | 533 | 502 | 26 | 1061 |
| 16 | DODOMA | 710 | 716 | | 1426 |
| 17 | RUKWA | 593 | 348 | 19 | 960 |
| 18 | LINDI | 430 | 462 | | 892 |
| | **TOTAL** | **11639** | **7349** | **873** | **19861** |

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2024 hoja 1017 zimepokelewa ambapo hoja 179 zitashughulikiwa na Baraza pamoja na kuwasilishwa kwa watoa huduma. Hoja zingine 838 ni hoja ambazo zimejirudia.

## 2.0 MASUALA YALIYOWASILISHWA NA KAMATI KISEKTA




### 3.0 Kushiriki katika kutoa elimu katika mikutano mbalimbali 2024

Kamati za watumiaji zimeweza kutoa elimu kwa njia mbalimbali katika Mikoa kama ifuatavyo;

**3.1 Kamati ya Mkoa wa Simiyu:** Kamati ya Mkoa wa Simiyu imetoa elimu kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano katika mkutano wa malezi na makuzi kwa watoto uliofanyika katika Wilaya ya Bariadi Mkoa wa Simiyu. Mkutano ulihudhuriwa na washiriki takribani 400 na Kamati kupata fursa ya kutoa elimu kuhusu Ulinzi wa Mtoto Mtandaoni na Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015. Aidha; wajumbe waliweza kugawa machapisho mbalimbali kwa washiriki kwa lengo la kuongeza wigo wa watu kusoma na kupata uelewa zaidi kuhusu sekta ya mawasiliano.

### 3.2 Mkoa wa Mjini Magharib

Sherehe za Mapinduzi mwaka 2023/24 zilitanguliwa na maonesho ya shughuli za biashara na kazi za taasisi mbalimbali za Serikali na za binafsi pamoja na

mashirika ya kitaifa na kimataifa. Zanzibar ilikua ikisheherekea miaka 60 ya Mapinduzi tangu mwaka 1964 Kauli Mbiu ilikuwa ni **“MIAKA 60 YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR TUIMARISHE UCHUMI, UZALENDO KWA MAENDELEO YA TAIFA LETU”**

Kamati ya Watumiaji wa Huduma na Bidhaa za Mawasiliano ya Mkoa wa Mjini Magharibi ilipata nafasi ya kuwakilisha Baraza la watumiaji wa huduma za Mawasiliano kwa wajumbe wa Kamati hiyo kushiriki siku zote za maonesho ambapo Rais wa Zanzibar Mh. Hussein Ally Mwinyi alifungua rasmi. Kamati ilipata fursa ya kutoa elimu na kupokea maoni ya watumiaji na takribani watumiaji 496 walifikiwa kupitia maonesho ya Mapinduzi.




*Wajumbe wa Kamati ya Mkoa wa Mjini Magharib wakishiriki katika maonesho ya Mapinduzi yaliyofanyika Zanzibar Januari, 2024*

**3.3** Kamati zingine zilizoendesha mikutano ya elimu, uhamasishaji na kupokea maoni ni pamoja na Kamati za watumiaji katika Mikoa ya Lindi, Mbeya, Pemba, Tabora, Iringa na Kigoma. Aidha Baraza liliendesha Mikutano 2 ya elimu kupitia Maadhimisho ya Siku ya Mtumiaji Duniani Jijini Dar es Salaam na Babati Mkoani Manyara. Maadhimisho ya Wiki ya Mtumiaji yalifanyika tarehe 15 Machi, 2024

na kufunguliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Katika maadhimisho hayo Wizara iliwakilishwa na Naibu Katibu Mkuu na Baraza liliwakilishwa na Mwenyekiti.